

Salim Ahmed Salim

OFISI YA DR. SALIM AHMED SALIM

Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Katibu Mkuu Mstaafu wa Jumuiya ya Muungano wa Nchi za Afrika (OAU)

26 Septemba, 2023

TOVUTI YA HIFADHI YA NYARAKA ZA DKT. SALIM AHMED SALIM KUZINDULIWA TAREHE 30 SEPTEMBER 2023

Tovuti ya hifadhi ya nyaraka za Dkt. Salim Ahmed Salim, mwanadiplomasia mashuhuri aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na, Katibu Mkuu wa Nane wa Jumuiya ya Muungano wa Nchi za Afrika (OAU) kuanzia mwaka 1989 – 2001, inatarajiwa kuzinduliwa tarehe 30 Septemba 2023, Jijini Dar es Salaam.

Mgeni rasmi wa tukio hilo atakuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi atashiriki. Wageni wengine ni pamoja na viongozi waandamizi kutoka kwenye sekta za umma na binafsi; viongozi wastaafu; na wawakilishi wa washirika wa maendeleo, asasi za kiraia, na taasisi za elimu ya juu.

Tovuti hii (www.salimahmedsalim.com) inajumuisha video, picha na nyaraka mbalimbali (kama vile hotuba, nakala za mawasiliano ya kimaandishi, na machapisho ya kitafiti) za Dkt. Salim. Inatoa ujuzi wa kipekee juu ya safari yake ya utumishi wa umma, na mchango wake katika mahusiano ya kimataifa na jitihada za ukombozi barani Afrika. Aidha, inaangazia mchango wa nchi za Afrika katika siasa za kimataifa katika kipindi cha mwaka 1960 hadi 2000. Imeandaliwa na familia ya Dkt. Salim kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na ndugu, jamaa na marafiki. Aidha, tovuti hii ambayo ni hifadhi ya matukio yaliyotengeneza maisha ya Dkt. Salim, na muhimu zaidi, hifadhi ya nukuu na nyaraka zake mwenyewe, inalenga kuimarisha historia ya Tanzania na ile ya Afrika.

Nyaraka za tovuti hii zitawavutia wale wanaotaka kuelewa mchango wa Tanzania na wa nchi nyingine barani Afrika katika historia ya dunia na siasa za kimataifa.

Ushiriki katika tukio hili ni kwa mwaliko pekee.

Imetolewa na,

Familia ya Dkt. Salim Ahmed Salim